

**HOTUBA YA MKURUGENZI MKUU WA TANTRADE KATIKA HAFLA  
YA KUFUNGA SIKU MAALUM YA WADAU WA SEKTA YA  
WAOKAJI TANZANIA ITAKAYOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA  
RASHID MFAUME KAWAWA, DOME KATIKA UWANJA WA  
MAONYESHO WA MWALIMU J.K. NYERERE**

**TAREHE 10 JULAI, 2022**

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Mama Tunu Mizengo Pinda, Mke wa  
Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu Msataafu wa  
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;  
Bi Fransisca Lyimo, Mwenyekiti wa Chama cha Waokaji  
Tanzania;  
Wakurugenzi wa Taasisi za Umma na Binafsi mliopo hapa;  
Watendaji wa Makampuni;  
Viongozi na wanachama wa Chama Cha Waokaji Tanzania;  
Wadhamini;  
Waandishi wa habari;  
Wananchi wote mliopo;  
Mabibi na Mabwana;***

## **Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

**Kwanza kabisa,** napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa Rehema kwa kutukutanisha mahali hapa tukiwa na afya njema.

**Pili** nitoe shukrani zangu kwako Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Mama Tunu Mizengo Pinda, kwa kukubali ombi la kuwa Mgeni Rasmi katika siku hii ya kuhitimisha Siku Maalum ya wadau wa Sekta ya Uokaji iliyofanyika sambamba na Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (46<sup>th</sup> DITF 2022), ilioandaliwa na Umoja wa Waokaji Tanzania (Tanzania Bakers' Association -TBA). **Tunakushukuru sana!**

### **Ndugu Mgeni Rasmi,**

Napenda nitoe pongezi kwa wote walioshirikiana na wadau wa sekta hii kupitia Umoja wao kwa namna moja au nyingine katika kuandaa siku hii ya leo. Na kwa kipekee, niishukuru na kuipongeza **Kampuni ya S.S.**

**Bakhresa** kwa namna ambavyo imejitoa kufanikisha Hafla hii.

### **Hongereni sana!**

### **Ndugu Mgeni Rasmi,**

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) ni Taasisi inayohusika na kuendeleza na kukuza Biashara nchini. Lengo kuu ni

kuimarisha ukuaji wa uchumi wa Tanzania kupitia Maendeleo ya Biashara. Pamoja na majukumu mengine, TanTrade ina jukumu la kuijengea uwezo Jumuiya ya wafanyabiashara juu ya namna bora ya kusimamia shughuli za Biashara na kukuza Biashara kupitia uendelezaji Bidhaa na kuongeza thamani ya Mazao. Vilevile, tunaratibu Maonesho ya Biashara, Misafara na Mikutano ya Wafanyabiashara ya ndani na nje ya nchi, Kufanya Tafiti za Masoko, Kukusanya, kuhariri na kutoa taarifa za Biashara pamoja na kudhibiti maonesho mbalimbali yanayofanyika nchini.

Hivyo, tunaona fahari kubwa kuwa sehemu ya walioshiriki bega kwa bega na umaja huu katika kuratibu na kuandaa Siku Maalum ya wadau wa Sekta hii wakati wa Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (46<sup>th</sup> DITF 2022) chini ya uratibu wa Umoja wa Waokaji Tanzania (TBA).

**Ndugu Mgeni Rasmi,**

TanTrade pia ilishirikiana na Wadau wa Sekta hii ya Uokaji katika kuzindua Umoja wao ambao utaleta tija katika Tasnia nzima ya Uokaji nchini. Kama mtakumbuka Maneno ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliposema

**“Ukitaka kufika unapokwenda nenda peke yako, lakini ukitaka kufika mbali, nenda na wenzako.”** Kauli hii ina maana na ina faida kubwa kwani katika umoja haki inapatikana, maendeleo yanaongezeka kwa sababu kutakuwa na kauli moja na watu wenye nia moja. Hivyo nawashauri wale ambao bado hawajajiunga katika umoja huu wajiunge kwa faida zaidi ili waweze kufika mbali.

Niwaombe wadau wote wa sekta hii na sekta zingine muendelee kushirikiana na TanTrade katika kuendeleza na kukuza Biashara zenu kupitia majukwaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na jukwaa hili la Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF).

Niwashukuru wote mlioshiriki katika siku hii maalum, nina imani mmefaidika na kujifunza mengi ambayo yatazidi kuwajenga vyema katika biashara zenu. Baada ya kusema hayo, naomba nikushurukuru tena mama **Tunu Mizengo Pinda** kwa kujumuika nasi siku ya leo na naomba sasa nikukaribishe uweze kuongea na hadhira hii. **Karibu sana!**

**Kazi iendelee!!**

**Asanteni kwa kunisikiliza.**